

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA KUMI NA TANO

23 APRILI, 2026



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA KUMI NA TANO – TAREHE 23 APRILI, 2026

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU (TAMISEMI):

171. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAK KHAMIS (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha Shule za Sekondari zinaondokana na Upungufu wa Vifaa vya Maabara.

OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MUUNGANO NA MAZINGIRA):

172. MHESHIMIWA SAIDI SALIM HAMAD (OLE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukuza na kuhifadhi Miti ya Mikoko ili kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi.

WIZARA YA MAJI:

173. MHESHIMIWA KHALID MUSSA NSEKELA (KYERWA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itachukua hatua za haraka za upatikanaji wa maji safi na salama katika Zahanati, Vituo vya Afya, Masoko na Mashuleni - Kyerwa.

WIZARA YA UJENZI:

174. MHESHIMIWA BAKARI BAKARI SHINGO (UKONGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Ujenzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati kwa dharura Barabara ya Nyerere maeneo ya Mombasa - Gongo la Mboto na eneo la Makaburi ya Kiltex.

**175. MHESHIMIWA GEORGE NATANY MALIMA
(MPWAPWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara kutoka Njiapanda ya Kongwa hadi Mpwapwa Mjini kwa kiwango cha lami.

176. MHESHIMIWA KAFITI WILLIAM KAFITI (ILEMELA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha ujenzi wa Barabara ya Airport - Kayenze km 34.

**177. MHESHIMIWA JANETH PETER PINDA (VITI
MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Barabara ya kiwango cha lami kutoka Kibaoni kupitia Majimoto hadi Inyonga.

WIZARA YA AFYA:

**178. MHESHIMIWA ADONIS ALFRED BITEGEKO
(MULEBA KASKAZINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, lini changamoto ya uwepo wa Maduka ya Dawa yasiyo na Vibali, Wataalamu, utoaji Dawa kiholela na uuzaji wa bidhaa zisizo rhusiwa itatatuliwa.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA NISHATI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

(Majadiliano yanaendelea)

**DODOMA
23 APRILI, 2026**

**BARAKA I. LEONARD
KATIBU WA BUNGE**